## Miadi ya Simu ya WIC www.healthvermont.gov/wicbyphone

Kama sehemu ya hatua zetu dhidi ya COVID 19, WIC itafanya miadi yote kwa simu ili kuzingatia juhudi za kujitenga na watu wengine katika Vermont. WIC imejitolea kuendelea kusaidia familia sasa na katika siku zijazo.

Maelezo yafuatayo yatasaidia familia za WIC kukamilisha miadi ya simu kwa mafanikio.

**Mambo ya Kutarajia**

Mfanyakazi wa Lishe wa WIC atakupigia simu kwa nambari ya simu uliyopea ofisi yako ya WIC iliyoko karibu. Tafadhali kumbuka kwamba huenda upokee simu kutoka kwa nambari ya kibinafsi badala ya nambari ya kliniki ya WIC. Utaulizwa mfululizo wa maswali ya kibinafsi, kwa hivyo tafuta sehemu yenye faragha, na ambapo hakuna kelele ili ukamilishe miadi. Mfanyakazi huyo wa WIC ataingiza maelezo hiyo kwenye kompyuta, kwa hivyo huenda mazungumzo yachelewe kiasi.

**Kuwa na Ufikiaji wa Intaneti**

Ikiwezekana, hakikisha kuwa ukurasa huu umefunguliwa ili iwe rahisi kufikia maelezo yanayoyohitajika ili ukamilishe maidi. Huenda pia uombwe utume kielektroniki picha za hati kwenye barua pepe salama ya ofisi yako iliyoko karibu. Mfanyakazi huyo wa WIC atakujulisha unayopaswa kufanya ili ukamilishe miadi kwa simu.

**Maelezo Mengine Yanayohitajika**

Ikiwa una vipimo vya kimo/urefu, uzani au uchunguzi wa chuma kutoka kwa ziara ya hivi karibuni ya daktari, unaweza kushiriki maelezo hayo na mfanyakazi huyo wa WIC. Ikiwa huna vipimo vyovyote vya hivi karibuni, miadi itakamilishwa bila maelezo hayo.

**Haki na Majukumu ya WIC**

Kama mshiriki wa kipindi cha Wanawake, Watoto wachanga na Watoto (WIC) ya Vermont, ninaelewa yafuatayo:

1. Muda wakufuzu kwa mshiriki hutofautiana kulingana na aina ya mshiriki:
    a. Wanawake wajawazito, mpaka muda wa wiki sita baada ya kujifungua;
    b. watoto wachanga/wanawake wanaonyonyesha, hadi mwaka wa kwanza wa kuzaliwa mtoto;
    c. watoto, kwa kipindi cha miezi kumi na miwili hadi umri wa miaka mitano, na
    d. kwa wanawake wasionyonyesha, miezi sita baada ya kujifungua.

2. Wakati mafunzo ya mtoto au watoto wangu yatakapokamilika, faida ya mpango huu wa WIC pia yatafikia kikomo.

3. Nitapokea maelezo kuhusu lishe na afya, ikiwa ni pamoja na elimu ya lishe, usaidizi wa kunyonyesha, vyakula vya WIC, na maelekezo kwa huduma zingine za afya.

4. Ili kuendelea kupokea manufaa ya WIC, endelea kuhudhuria mafunzo yote na kushiriki elimu ya lishe yote.

5. Nina haki ya maelezo ninayotoa kwa mpango wa WIC kuhifadhiwa kwa usiri.
Ninaelewa kwamba maelezo ya mshiriki wa kipindi cha WIC yanaweza kushirikiwa na mipango ifuatayo: Mpango wa Kutembelea Watu Nyumbani, Huduma za Malezi, Chanjo, Mfumo wa Ufuatiliaji wa Utathmini wa Hatari za Mimba (PRAMS). Sahihi yangu ya kielektroniki kwenye uthibitishaji wa Mpango

wa WIC itatumika kama idhini ya kutoa maelezo kwa kushiriki maelezo. Idhini nyingine tofauti ya kutoa maelezo yangu kwa huluki nyingine yoyote inahitajika.

6. Kamishna wa Afya wa Vermont anaweza kuidhinisha matumizi na kutolewa kwa maelezo kuhusu ushiriki wangu katika WIC kwa madhumuni yasiyo ya WIC. Maelezo kama haya yatatumiwa na ofisi za eneo na za jimbo za WIC na kwa mipango iliyoorodheshwa hapo juu kwa madhumuni TU ya usimamizi wa mpango, kuratibu manufaa katika mipango mingine na kuboresha huduma na shughuli za WIC.

7. Maelezo kuhusu tabaka/kabila yanakusanywa kwa ajili ya mahitaji tu ya kuripoti takwimu na hayataathiri kushiriki kwangu katika Mpango wa WIC. Viwango vya ustahiki na ushiriki katika Mpango wa WIC ni sawa kwa kila mtu, bila kujali kabila, rangi, asili ya nchi, umri, ulemavu, au jinsia.

8. Wafanyakazi wa WIC wanaweza kuthibitisha maelezo ninayotoa. Kama nimetoa maelezo ya uongo, huenda nisipate manufaa ya WIC; huenda nikahitajika kulipa pesa za vyakula vya WIC ambazo tayari vimenunuliwa; na ninaweza kushtakiwa chini ya sheria za jimbo na nchi.

9. Kama nitahama kwenye eneo la Vermont, ninaweza kuomba Uthibitishaji wa Uthibitisho (VOC) ili niendelee kupata manufaa ya WIC katika jimbo mpya.

**Haki za Mshiriki wa Mpango wa WIC:**

- Kama sikubaliani na uamuzi wowote unaothiri ustahiki au manufaa yangu kutoka WIC, nina siku sitini (60) kuanzia tarehe ya kutoa maelezo ili kukata rufaa na kuomba kikao cha kusikilizwa kwa haki ili kuwasilisha sababu za pingamizi na mimi au na mwakilishi wangu, kama vile jamaa/rafiki/mshauri wa kisheria au msemaji mwingine.
- Maelezo ya kuomba kikao cha kusikilizwa kwa kesi yanaweza kupatikana kutoka kwa ofisi zozote za eneo za WIC au katika Ofisi za ya Jimbo ya WIC katika: Idara ya Afya ya Vermont, Mpango wa WIC, 108 Cherry Street, Sanduku la Posta 70, Burlington, VT 05402-0070. Unaweza pia kutupigia simu ili kuomba kikao cha kusikilizwa kwa kesi yako kupitia 1-800-649-4357.
- Unaweza kuomba uendelee kupata manufaa ukisubiri matokeo ya rufaa yako ya kusikilizwa kwa kesi. Ombi lazima liwasilishwe ndani ya siku 15 kuanzia tarehe ya Taarifa ya Kutostahiki. Hata hivyo, huwezi kuendelea kupata manufaa baada ya kipindi cha uthibitishaji wa mshiriki.
- WIC ni mpango ya nafasi sawa. Kama ninaamini kuwa nimebaguliwa kwa sababu ya mbari, rangi, asili ya kitaifa, jinsia, umri au ulemavu, ninaweza kuwasiliana na Katibu wa Kilimo, Washington, DC, 20250 moja kwa moja, au kuomba usaidizi kutoka kwa wafanyakazi wa WIC kufanya hivyo.

**Majukumu ya Mshiriki katika Mpango wa WIC:**

1. Ili kuepuka hasara ya kupoteza manufaa ya WIC, ni lazima nihudhurie miadi yote ya WIC.
2. Kama sitaweza kuhudhuria miadi ya WIC, nitawajulisha mapema kwa simu ili kuratibu tena. Kama nitakosa hatua ya uthibitishaji tena au nitakosa kuhudhuria darasa la elimu ya lishe bora, manufaa ya WIC yanaweza kupunguzwa.
3. Nitawaarifu wafanyakazi wa WIC iwapo nitabadilisha anwani yangu au kuhamia mji au jimbo lingine ili manufaa yangu ya WIC yaweze kuhamishwa hadi wilaya au jimbo lingine.
4. Vyakula vya WIC ni kwa ajili ya mwanafamilia anayeshiriki. Sitauza au kutoa manufaa yangu ya WIC kwa mtu mwingine yeyote na nitawasiliana na WIC kama nitahitaji kubadilisha manufaa yangu ya vyakula.
5. Ubadilishaji wote wa fomyula/vyakula vya kimatibabu lazima ufanyike kwenye ofisi za WIC. Fomyula yoyote ya mtoto mchanga ambayo haijatumika, lazima irudishwe kwenye ofisi za WIC.

6. Nitaweka kadi yangu ya WIC mahali salama, na sitatoa nambari yangu ya kitambulisho binafsi kwa mtu yeyote isipokuwa mtu ambaye anafanya ununuzi wa WIC kama mkuu wa ziada wa nyumbani kwangu au kwa niaba yangu.
7. Kama kadi yangu ya Vermont WIC itapotea au kuibiwa, nitaripoti hili mara moja kwenye ofisi za WIC. Ninaelewa kwamba inawezekana manufaa ya mwezi wa sasa hayatafidiwa.
8. Naelewa kuwa manufaa ya WIC yanapaswa kununuliwa tu katika maduka yaliyoidhinishwa na WIC kwa mwezi uliyotengwa na kutumiwa na mshiriki aliyetengewa, na kwamba manufaa yanayosalia hayawezi kutumika katika miezi inayofuata.
9. Ni wajibu wangu kutoa mafunzo kwa mkuu wa ziada wa nyumba yangu au wakala wangu kutumia kadi yangu katika duka.
10. Ninawajibu wa kuhakikisha kuwa mnunuzi wangu mbadala anatimiza majukumu haya sawa.

Ubatilishaji, usimamishaji, ushtaki, na urejeshaji wa fedha unaweza kutokea kwa:

A. Matumizi mabaya ya manufaa ya WIC kama vile kubadilisha/kuuza au kunuia kuuza kadi ya Vermont WIC au bidhaa za vyakula zilizonunuliwa kupitia manufaa ya WIC kwa maneno, chapisho, mtandaoni, au kwa njia nyingine yoyote kwa fedha taslimu, mkopo, au bidhaa zisizo za vyakula.
B. Kununua/kupokea vyakula visivyo katika Orodha ya WIC ya Vyakula Vilivyoidhinishwa.
C. Dhuluma ya kimwili, tishio la dhuluma ya kimwili au matusi kwa wafanyakazi wa WIC au wa duka la vyakula.

Maelezo ya fedha na ustahiki ambayo nimetoa ni ya kweli kulingana na ufahamu wangu ikiwa ni pamoja na mapato katika nyumba, idadi ya watu katika nyumba, anwani, nyaraka za utambulisho na maelezo kuhusu hali ya afya na lishe. Nitawajulisha wafanyakazi wa WIC mara moja kuhusu mabadiliko yoyote. Kwa kutoa sahihi yangu ya kielektroniki katika mfumo wa VT WIC Ceres, nathibitisha yafuatayo:

1. Kibali na ufahamu wangu kwa taarifa zilizotajwa hapo juu.
2. Nimeshauriwa kuhusu, naelewa, na nimesoma na kupewa nakala ya Haki na Majukumu ya Mshiriki wa Mpango wa VT WIC na Taarifa ya Desturi za Faragha.

Kwa mujibu wa sheria ya haki za raia za Nchi na sera na sheria za haki za raia za Idara ya Kilimo ya Marekani (USDA), USDA, Mashirika yake, maofisi, na wafanyakazi, na taasisi zinazoshiriki au kusimamia mipango ya USDA zimepigwa marufuku kubagua kwa misingi ya mbari, rangi, taifa ya asili, jinsia, ulemavu, umri, au kuadhibu au kulipiza kisasi kwa ajili ya shughuli ya awali haki za raia katika mpango au shughuli yoyote inayotekelezwa au kufadhiliwa na USDA. Watu walio na ulemavu ambao wanahitaji njia mbadala za mawasiliano kwa ajili ya maelezo ya mpango (k.m., Breli, machapisho makubwa, kanda ya sauti, Lugha ya Ishara ya Marekani nk.), wanapaswa kuwasiliana na shirika (katika Jimbo au eneo) ambapo walituma maombi ya manufaa. Watu ambao ni viziwi, walio na ugumu wa kusikia au walio na matatizo ya kuzungumza wanaweza kuwasiliana na USDA kupitia Huduma ya Nchi ya Kuhamisha Simu kupitia (800) 877-8339. Zaidi ya hayo, maelezo ya mpango yanaweza kutolewa katika lugha zingine kando na Kiingereza.

Ili kuwasilisha malalamiko ya ubaguzi katika mpango, kamilisha Fomu ya Malalamiko ya Ubaguzi ya Mpango wa USDA, (AD-3027) inayopatikana mtandaoni kwenye anwani : http://www.ascr.usda.gov/complaint_filing_cust.html (kiungo kinaelekeza nje), na katika ofisi yoyote ya USDA, au andika barua kwa USDA ukitoa maelezo yote yanayoombwa katika fomu. Ili kuomba nakala ya fomu ya malalamiko, piga simu kwa (866) 632-9992. Wasilisha fomu au barua yako uliokamilisha kwa USDA kupitia:

(1) Barua: Idara ya Kilimo ya Marekani
Ofisi ya Mratibu Msaidizi wa Haki za Raia

1400 Independence Avenue, SW
Washington, D.C. 20250-9410;

(2) Faksi: (202) 690-7442; au

(3) Barua pepe: program.intake@usda.gov.

Taasisi hii ni mtoa huduma wa nafasi sawa.

**Raslimali za Miadi**

Kwa maswali na maelezo yanayohusiana na kunyonyesha, tembelea Ukurasa kuhusu Uyonyeshaji wa WIC

Kwa maelezo kuhusu vyakula vya WIC, tembelea Ukurasa wa Kufanya Ununuzi na WIC , angalia Mwongozo wa Vyakula vya WIC Vermont na Mwongozo wa Ununuzi na Mpango wa WIC

Ili ukamilishe shughuli za Kielimu za Lishe za mtandaoni, tembelea WICHealth.org